**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**

*Dar es Salaam*
*01 Machi, 2026*

Baruapepe: press@ikulu.go.tz

# TAARIFA KWA UMMA

## RAIS SAMIA AKUTANA NA UJUMBE WA TAASISI YA KEEP A CHILD ALIVE, IKULU DAR ES SALAAM

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, leo amekutana na ujumbe wa taasisi ya *Keep a Child Alive (KCA)* ukiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wake, Bw. Antonio Ruiz-Giménez, Jr., Ikulu Dar es Salaam.

Mazungumzo hayo yalilenga kuimarisha ushirikiano katika kuboresha huduma za uzazi na afya ya mama na mtoto nchini, na yameweka msingi wa ujenzi wa wodi 27 za kisasa za kulelea watoto njiti Tanzania Bara na Zanzibar, zitakazojengwa kwa viwango vya kimataifa.

Mpango huo utatekelezwa kwa ushirikiano na taasisi ya *Doris Mollel Foundation* na unakusudia kuimarisha miundombinu ya afya ya uzazi, kuongeza upatikanaji wa vifaa tiba na kuchangia kupunguza vifo vya akina mama na watoto wachanga wanaozaliwa kabla ya wakati (watoto njiti).

Rais Dkt. Samia amesema Tanzania imepiga hatua kubwa katika kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, kutoka vifo 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2016 hadi 104 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2022. Katika kipindi hicho, vifo vya watoto chini ya miaka mitano vimepungua kwa asilimia 36, kutoka 67 hadi 43 kwa kila vizazi hai 1,000.

Ameongeza kuwa, mafanikio hayo yametokana na uwekezaji katika ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya jirani na wananchi, kuongeza ajira za watumishi wa afya na kuimarisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba vya kisasa.

Hatahivyo, amebainisha kuwa changamoto bado ipo katika kupunguza vifo vya watoto wachanga kutokana na upungufu wa wodi maalum za watoto wachanga, na kubainisha mpango mkakati wa Serikali, katika kukabiliana na hali hiyo, wa kujenga wodi 15 katika

hospitali za mikoa na wodi 20 katika hospitali za wilaya kwa viwango vinavyokidhi hadhi ya kimataifa.

Ushirikiano baina ya Serikali na *Keep a Child Alive* unalenga kuharakisha utekelezaji wa azma hiyo kupitia ujenzi wa miundombinu bora, uwekezaji katika vifaa vya kisasa vya kulelea watoto njiti *(incubators),* mafunzo kwa wataalamu wa afya na usimamizi madhubuti wa rasilimali za afya ili kufikia malengo ya pamoja yaliyokusudiwa.

Rais Dkt. Samia ameeleza utayari wa kuwezesha utekelezaji wa mpango huo kupitia uratibu wa kitaalamu, upatikanaji wa maeneo ya ujenzi na ujumuishaji wa vituo hivyo katika mfumo rasmi wa afya ili kuhakikisha uendelevu wake.

Kwa upande wake, Bw. Ruiz-Giménez, Jr. amemshukuru Rais Dkt. Samia kwa ukaribisho alioupata na kueleza utayari wa KCA kuendelea kushirikiana na Tanzania katika kuimarisha huduma za afya, hususan katika afya ya mama na mtoto.

Rais Dkt. Samia, ambaye pia ni Kinara wa Umoja wa Afrika katika Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto, amesema ushirikiano huo utaongeza upatikanaji wa huduma za uzazi salama, kupunguza vifo vinavyoweza kuzuilika na kuimarisha mfumo wa afya ya mama na mtoto nchini.

**TAARIFA KWA MHARIRI**

Taasisi ya *Keep a Child Alive (KCA)* ilianzishwa mwaka 2003 na msanii na mwanaharakati wa kimataifa wa haki za binadamu, Alicia Keys. Taasisi hiyo hutoa huduma za afya na msaada wa kijamii kwa watoto na familia zilizo katika mazingira magumu duniani.

Nchini Tanzania, KCA kwa kushirikiana na taasisi ya *Doris Mollel Foundation* imefanikisha ujenzi na uimarishaji wa wodi ya watoto wachanga katika Hospitali ya Wilaya ya Kwimba, mkoani Mwanza.



Bakari S. Machumu
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu